



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

**TANGAZO LA ZABUNI**  
**KWA AJILI YAUKARABATI WA MIUNDOBINU OFISI ZA HALMASHAURI**  
**Tarehe 24/11/2022**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilayani Biharamulo chini ya sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia **Wananchi, Makampuni, Taasisi na Vikundi mbalimbali** kuomba zabuni katika **UKARABATI WA MIUNDOBINU OFISI ZA HALMASHAURI** kama ifuatavyo:-

<b>Fungu Na.</b>	<b>Maelezo</b> <i>[Orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji]</i>
LGA/032/2022-2023/HQ/NCS/ 1/LOT.9	Fundi Ujenzi Ukarabati wa MiundoMbinu Ofisi za Halmashauri
LGA/032/2022-2022/HQ/G/10	Usafirishaji na uuzaji wa madini ya ujenzi (Mchanga, na Kokoto ), Tofali za Block na Mbao

**MASHARTI MUHIMU YA ZABUNI**


- Awe Mtanzania mwenye Kitambulisho cha Mpiga Kura au cha Taifa au Leseni ya Udereva au Hati ya kusafiria na apatikane kirahisi wakati wa kutekeleza kazi.
- Awe na utambulisho kutoka ofisi ya kijiji/Mtaa au kata anayoishi
- Awe amesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
- Awe tayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa
- Awe na busara ya kusikiliza ushauri wa kitaalamu wa ujenzi
- Fundi awe na uwezo wa kukarabati, kumaliza na kukabidhi kazi kwa muda atakaopewa
- Waombaji wa uuzaji wa madini ya ujenzi, Tofali na Mbao wawe na Leseni hai za biashara
- Waombaji wa ufundi wa Ukarabati wa Miundombinu Ofisi za Halmashauri waambatanishe uthibitisho wa uzoefu aliyonawo.
- Waombaji wa uuzaji wa madini ya ujenzi, Tofali na Mbao wawe na uwezo wa kutoa risiti ya EFD ya kupokea malipo (kukiri mapokezi ya fedha) au uthibitisho wa kutotoa EFD .



- j) Muombaji wa uuzaji wa madini ya ujenzi ni lazima awe na gari lenye ujazo wa kuanzia 4.5 hadi 16.
- k) Waombaji wa kazi ya ufundi wawasilishe mpango kazi wa njinsi ambavyo atakamilisha kazi ya Ukarabati kwa muda usiozidi Siku 21
- l) Awe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali watu na vitendea kazi muhimu
- m) Mwombaji ahakikishe fomu zote za maombi ya zabuni zimejazwa kwa uhakika bila kukosewa.
- n) Maombi yote yaambatanishwe na barua ya maombi ya zabuni yenye taarifa ya njia za mawasiliano kama vile namba za simu, Majina mawili ya Wadhamini, barua pepe au anwani za makazi pamoja na risiti ya malipo ya maombi kwa kila ombi la zabuni itakayotolewa katika ofisi ya **Ofisi ya Manunuzi na Ugavi iliyopo katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.**
- o) Vitabu vya nyaraka za nukuu ya bei vinapatikana katika **Ofisi ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi (PMU) kwa ada ya maombi ya Tsh 30,000/= zitazolipwa baada ya kupewa control number kutoka Idara ya fedha na Biashara ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.**
- p) Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyo kamilika, maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa na zoezi la uchambuzi wa kumpata mzabuni.
- q) Maombi yanatakiwa kufungwa kwenye bahasha na kuonesha aina ya zabuni inayoombwa bila kuwa na viashiria vyovyote inakotoka na yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO  
S.L.P. 70,  
BIHARAMULO.**

Muda wa mwisho wa kupokea Maombi (Kotesheni zilizojazwa) ni **saa nne (4) kamili asubuhi (4:00)** (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **30/11/2022** siku ya **Jumatano na zabuni zitafunguliwa saa 4:30** katika **Ukumbi wa Mikutano** wa Halmashauri ya **Wilaya ya Biharamulo**. Waombaji au wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi.



.....  
**INNOCENT M. MUKANDALA  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BIHARAMULO**